Jamhuri ya Kenya

# Wizara ya Ardhi, Kazi za Umma, Nyumba na Ustawi wa Miji

## Idara ya Kitaifa ya Ardhi na Mipangilio ya Ardhi

## NOTISI KWA UMMA

### MRADI WA KUSAFISHA MITO YA NAIROBI - URATIBU WA MIPAKA YA HIFADHI ZA MITO, CHEMCHEMI NA VIJITO VILIVYO KANDO YA MITO YA NAIROBI

Kulingana na **Waraka wa Baraza la Mawaziri - Nambari 6 ya 2024, uliotolewa tarehe 30 Aprili 2024**, umma unafahamishwa kuhusu kuanza kwa shughuli za kukamilisha **uratibu** na **uwianishaj**i wa mipaka ya ardhi iliyo kando ya mito ya Nairobi (**Mto Nairobi, Mathare, Ngong, Miotoni, Mokoyeti, Mbagathi, Ruaka, Gethathuru, Kibagare na vijito vyake**) kuanzia katika vyanzo vyake.

Umma unafahamishwa shughuli hiyo itafanywa kulingana na **kifungu cha 5, 62, 66 na 69 cha Katiba ya Kenya - 2010, Sheria ya Ardhi, 2012, Sheria ya Maji, 2016, Sheria ya Utafiti, Sura ya 299, Sheria ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira, 1999 EMCA Sura ya 387, Sheria ya Ardhi na Mipangilio ya Matumizi ya Ardhi (PLUPA), 2019** – pamoja na kanuni husika zilizo kwenye **Kanuni [Jumla] za Ardhi na Mipangilio ya Matumizi ya Ardhi (Vibali na Udhibiti wa Ustawi), 2021** kuhusu ulinzi, mipangilio, na usimamizi thabiti wa hifadhi za mito, vinamasi na chemchemi.

Shughuli hii ya kuratibu mipaka, itafanywa na kikosi kutoka katika **Mashirika Mbalimbali**, kikiongozwa na Mkurugenzi wa Mipangilio ya Ardhi na Mkurugenzi wa Utafiti – Idara ya Kitaifa ya Ardhi na Mipangilio ya Ardhi, Idara ya Kitaifa ya Usalama wa Ndani na Uratibu wa Kitaifa kupitia kwa Maafisa wa Utawala wa Serikali ya Kitaifa (NGAO), Mamlaka ya Rasilimali za Maji (WRA), Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA), Serikali ya Kaunti ya Nairobi, na Tume ya Mito ya Nairobi.

Shughuli hiyo **itahusisha Mito yote 3 ya Nairobi (Mto Nairobi, Ngong na Mathare), Mto Miotoni, Mto Mokoyeti, Mto Mbagathi, Mto Ruaka, Mto Gethathuru, Mto Kibagare** na vijito vyake. Pia litahusisha vinamasi na chemchemi.

**Shughuli hiyo itaanza tarehe 22 Desemba 2025.**

Umma unahitajika kuzingatia na kufuata mambo yafuatayo:

1. Katiba ya Kenya, 2010, inaelekeza kwamba uratibu wa mipaka ya hifadhi za mito utazingatia maeneo yenye maji mengi na maji machache kwenye mto na sio katikati ya mto.
2. Notisi hii inatumike kama ombi la ushirikiano katika kufikia nyumba zilizo kando ya Mito yote ya Nairobi na vijito vyake. Maafisa walioidhinishwa na vikosi vya kiufundi watahitaji kuingia ili kufanya uchunguzi, ukaguzi, na shughuli za uratibu wa mipaka.
3. Wamiliki na wapangaji wa nyumba hizo wanahimizwa kurahisisha shughuli hiyo kwa kuruhusu vikosi hivyo kuingia katika nyumba hizo bila shida yoyote.
4. Baadaye katika harakati hii, wamiliki halali na wapangaji wa nyumba zilizo karibu na Mito ya Nairobi wanaweza kuombwa kuwasilisha – nakala za umiliki, zikiwemo – hati miliki na cheti cha upimaji, vyeti vya kukodisha, idhini zote za ujenzi na mipaka, uratibu wowote kando ya mito, vikiwemo vibali vya matumizi na vibali kutoka kwa idara husika za Mipangilio na Ustawi wa Jiji au Kaunti, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) na Mamlaka ya Rasilimali za Maji (WRA) (iliyojulikana hapo nyuma kama Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji –WRMA). Nyaraka zinazohitajika zinapaswa kuwasilishwa ndani ya **siku kumi na nne (14)** baada ya maombi hayo kufanywa.
5. Kuhakikisha kwamba hakuna shughuli zozote zilizopigwa marufuku chini ya Sheria ya Maji (2016) na Kanuni (Jumla) za Mipangilio ya Matumizi ya Ardhi (Vibali na Udhibiti wa Ustawi), 2021 zinazofanywa ndani ya hifadhi za mito, vinamasi na chemchemi.
6. Pale ambapo watu wanaishi katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko, kuna nyumba zisizo halali, zisizoruhusiwa, kuna uvamizi na matumizi ya ardhi yasiyofaa katika ardhi hiyo, kuondolewa kwao kutafanywa kulingana na sheria. Hii inajumuisha kufuata utaratibu unaofaa, ushirikishaji wa umma, utoaji wa notisi zinazofaa, na kuzingatia haki za walioathiriwa.

Mhe Alice Wahome EGH

**WAZIRI**
**Katika Wizara ya Ardhi, Kazi za Umma, Nyumba na Ustawi wa Miji**
**S.L.P. 30119–00100, Nairobi**